# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 10 Juni, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE.ADAM K. MALIMA):**

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2013/2014 *(The Annual Report of The Bank of Tanzania for the year 2013/2014)*.

*The Annual Performance Evaluation Report for the Financial Year 2013/2014.*

**SPIKA:** Ahsante. Katibu!

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 178

### Ujenzi wa Daraja na Barabara ya Ilolangula-Isebya-Nyashinge-Mto Nyikonga-Rwamgasa

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Barabara ya Ilolangula-Isebya-Nyashinge - Mto Nyikonga hadi Rwamgasa ni kiungo muhimu cha shughuli za kiuchumi kati ya Wilaya za Mbogwe na Geita:-

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza fedha zaidi katika kujenga na kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika mto Nyikonga?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI MKUU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mbunge wa Mbogwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Ilolangula –Isebya - Nyashinge - Mto Nyikonga - Rwamgasa yenye urefu wa kilomita nne, ulianza mwezi Februari, 2015 kutokana na barabara hiyo kutengewa jumla ya shilingi milioni 150 katika mwaka wa fedha 2014/2015. Kati ya kiasi hicho cha fedha, fedha ambazo zimeshatolewa ni kiasi cha shilingi milioni 50 na zimetumika kwa kazi zifuatazo:-

(i) Kusafisha eneo la barabara umbali wa kilomita nne;

(ii) Barabara kulimwa kwa *grader* umbali wa kilomita nne;
(iii) Kuinua tuta la barabara umbali wa kilomita moja;

(iv) Kuweka changarawe mita za ujazo 300;

(v) Kuweka kalvati mistari minne; na

(vi) Kusomba *trips* 20 za kokoto na 15 za mawe kwa ajili ya ujenzi wa daraja.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali kupitia Hazina imeitengea Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, jumla ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja na barabara. Hivyo, kiasi cha fedha hizo kitatumika katika ujenzi wa Mto Nyikonga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masele swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, halmashauri walikadiria kwamba ujenzi wa daraja pamoja na utengenezaji wa ile barabara ingegharimu karibu shilingi milioni 399 na Serikali ikatoa shilingi milioni 150. Nataka kujua tu, ni lini sasa

Serikali itatoa fedha kiasi hicho ambacho kimesalia ili kusudi daraja lile liweze kujengwa na watu waweze kusafiri kwa amani? Maana kuna watu wanakufa pale, mvua zinapokuwa zimenyesha mto ukajaa, wanapita pale kwa kutumia mitubwi ya magome ya miti mwisho wanadumbukia mle wanakufa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri atakubali kufanya ziara huko Mbogwe, nimpeleke eneo la tukio akaone athari inayopatikana pale kwenye mto, pale ambapo watu wamekuwa wakiathirika? Aone ushuhuda huo labda pengine ataishauri Serikali iweze kutufikiria kwa kiwango ambacho kinastahili. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, moja, Serikali ina nia ya dhati kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa na inafahamika kabisa kwamba eneo hili huwa linawaathiri wananchi wengi wa Mbogwe kufika katika maeneo ya kilimo na kadhalika.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba kwanza ile shilingi milioni 150 inapatikana yote, ikipatikana maana yake ni kwamba tutakuwa tumemaliza tatizo kubwa la barabara ile.

Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja, kama nilivyosema kwamba fedha zile zilizotengwa kwa ajili ya madaraja na barabara kwa mwaka 2015/2016 zile shilingi milioni 300, mtapunguza kidogo kwa ajili ya kujenga hilo daraja. *Alternative* nyingine ni kuomba maombi maalumu ya fedha za maendeleo, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, mara nyingi tunafanya *allocation* kwenye maeneo magumu kama hayo. Kwa hiyo, njia zote hizi tatu zitatuwezesha kutengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu ziara, nitawasiliana na Mheshimiwa Mwanri ili nihakikishe kwamba anafika Mbogwe na katika hilo eneo la Mto Nyikonga ili aweze kujionea mwenyewe na kutia msukumo zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali swali la nyongeza.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kuna barabara za namna hii kwenye miji mingi ambazo ziliahidiwa mwaka 2010, kama Mji wa Kibondo, Mji wa Karatu, Mji wa Kondoa, kote kote wakati mnaomba kura CCM, mliahidi kujenga barabara lakini hamjajenga mpaka sasa hivi. Sasa swali, mtawaambia nini wananchi baada ya kutoa ahadi hewa kwenye miji mingi, hiyo ni michache tu nimeisema, mtawaambia nini mwaka huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu, swali rahisi kweli hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. OFISI YA WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama ametembea miji yote ambayo tumeahidi, lakini bora angekuwa *specific* kwa Kibondo au kwa eneo lake, ni kwamba ahadi hizo zitatimizwa kama tulivyopanga na hizo sehemu nyingine anazosema kama Kondoa na kwingineko, barabara hizo zinajengwa. Labda kwenye Jimbo lake ndipo bado hakujajengwa lakini sehemu nyinginezo kama Kondoa na miji mingine mingi tu, hata mji wangu wa Ulanga, barabara zimejengwa.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Mendrad Kigola.

Na. 179

**Maeneo Yaliyochukuliwa Mufindi**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia maeneo mbadala wananchi wa vijiji vya Sawala, Kihanga, Luhunga, Mkonge, Igoda, Mininga, Kitasengwa, Iyegeya, Kilolo, Ihomasa na Udumka ambao maeneo yao yalichukuliwa na kampuni za *MPM, Uniliver Tea* na Idara ya Misitu kwa ajili ya kilimo cha chai na upandaji miti na kusababisha wananchi hao kukosa maeneo kwa ajili kilimo, ufugaji na ujenzi wa nyumba za kuishi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI MKUU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba tarehe 6/10/1955, Chifu Adam Sapi Mkwawa wa kabila la Wahehe, aliingia mkataba wa makubaliano na Serikali ya Kikoloni kuwaondoa wananchi katika maeneo yaliyoamuliwa kupandwa miti katika Msitu wa Taifa wa *Sao Hill*. Kufuatia tathmini iliyofanyika mwaka 1951, wananchi waliotwaliwa maeneo yao walifidiwa kwa kupewa nusu ekari kwa kila kaya kwa ajili ya ujenzi wa makazi pamoja na ekari 30 kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji. Aidha, kumbukumbu hizo zinaonyesha kwamba, mwaka 1953/1954, jumla ya wananchi 83 wa Kijiji cha Kasanga, Sawala, Ikweha, na katika Kijiji cha Kihanga walilipwa fidia, kati ya shilingi 70 na shilingi 470 kila mmoja ili kupisha eneo kwa ajili ya kupandwa miti.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vijiji yaliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha karatasi yaani *Mufindi Paper Mill* kati ya mwaka 1978 na 1982,

yalikuwa maeneo ya wazi, nje ya makazi ya wanakijiji na hayakuwa yanatumiwa na mtu yeyote isipokuwa eneo la makaburi 10 ambayo yalifanyiwa uthamini na wenye makaburi hayo walilipwa fidia ya shilingi 5,800 kama fidia ya gharama ya kuhamisha makaburi katika eneo hilo. Aidha, wananchi wachache waliokuwa ndani ya eneo lililotwaliwa na kampuni ya *Uniliver Tea* kati ya mwaka 1931 na 1959, walihamia vijiji vya jirani ambako walipata maeneo mpya ya makazi na kuendelea na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kutoa mashamba hayo kwa kampuni ya *Uniliver* ulikuwa kuwekeza kwenye kilimo cha chai na kufungua kiwanda cha chai, kujenga kiwanda cha karatasi na upandaji wa miti kwa ajili ya kulisha kiwanda cha karatasi na kuzalisha nishati kwa ajili ya kiwanda. Aidha, shamba la miti la *Sao Hill*, kama ilivyokuwa mashamba mengine ya Serikali, lilianzishwa kwa madhumuni ya:-

(a) Kupunguza utegemezi wa misitu ya asili katika chanzo cha malighafi ya miti kwa matumizi mbalimbali;

(b) Kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji;

(c) Kutoa malighafi ya miti kwa ajili ya viwanda; na

(d) Kuwapatia ajira wananchi wa Wilaya ya Mufindi, pia ni chanzo cha mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika ngazi ya wilaya na mkoa, inatambua mahitaji makubwa ya ardhi yaliyoanza kujitokeza wilayani Mufindi kutokana na ongezeko kubwa la watu, mahitaji makubwa ya ardhi ya kupanda miti na uelewa mkubwa wa thamani ya ardhi. Mahitaji hayo yanafanya kila mwananchi kutafuta ardhi, kwani hata maeneo ya Msitu wa Taifa wa *Sao Hill* yamekuwa yakivamiwa na wananchi wa vijiji vinavyozunguka misitu na kusababisha migogoro ya ardhi kati ya Msitu wa Taifa wa *Sao Hill* na vijiji vinavyozunguka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigola swali la nyongeza.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri aliyojibu, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshakubali kwamba kuna ongezeko kubwa la watu na mashamba yalipimwa miaka ya zamani sana, miaka ya 1951 na sasa hivi idadi ya watu imekuwa kubwa na watu hawana sehemu kabisa ya kujenga. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu yale maeneo ya misitu ambayo yamekaa, kwa mfano, pale Udumka, Ihomasa na Kitasengwa, kuna

maeneo yamekaa tu, wananchi waliondolewa pale, kwa nini wasirudishiwe maeneo yale wananchi ili waweze kufanya shughuli zao zao za kila siku?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, *MPA* pale Sawala, kuna sehemu imebaki tu, walipanda miti ambapo wananchi wangeweza kujenga nyumba pale. Je, Serikali haiwezi kuongea na mwekezaji huyu ili aweze kupisha pale wananchi waweze kujenga nyumba za kuishi pale? Kwa sababu hakuna kabisa sehemu za kujenga nyumba, wananchi wanapata shida sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri na watu wengi tulikuwa hatujui historia ya *Sao Hill* na maeneo hayo, yalikuwa ni maamuzi ya busara ambayo wazee wetu waliyatoa na sasa hizi tunafaidika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na uelewa wa wananchi, sasa hivi kila mmoja anatambua umuhimu wa ardhi na ni ukweli usiopingika kwamba idadi ya wananchi pale Mufindi sasa hivi imeongezeka. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tutakaa kuangalia maeneo hayo ya wazi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema, tutakaa kwa pamoja Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na TAMISEMI, kuangalia je, maeneo hayo ya wazi tunaweza tukayabadilisha matumizi tukawapa wananchi au namna gani. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifanya hilo halafu tumpa majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba miti ni muhimu kwa ajili ya uhai wa taifa letu lakini kuna maeneo mengi ambayo migogoro inatokea kutokana na wananchi kutonufaika na ile maliasili iliyokuwepo katika eneo lao. Kwa mfano, tunajua tuna tatizo kubwa sana la madawati hapa nchini, sasa ili kuhakikisha wananchi wanatoa ushirikiano katika haya mashamba ya miti, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwenye shule za sekondari na msingi za maeneo hayo mfano Mufindi kwa kaka yangu Kigola, Kilombero, Sengerema wanawapatia madawati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI) (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama kuna maliasili wale watu au vijiji vinavyozunguka vinastahili kufaidika na hiyo maliasili, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo ni la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini lazima sheria zifuatwe, kisheria tunasema kwamba kama kuna tatizo la madawati na sehemu hii ina rasilimali za miti, ni vyema wananchi wa sehemu husika wakaomba kibali maalumu kwa Ofisi ya Maliasili Wilaya au Mkoa au Taifa cha kukata miti ili waweze wakapatiwa hicho kibali wakate miti kwa ajili ya madawati na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi, wengi wana *misuse* hicho kibali, wanachukua hicho kibali halafu wanafanya kwa manufaa mengine na siyo yale ambayo yanatakiwa. Tukifuata *procedure,* vijiji vingi vimefaidika na niwaombe tu wananchi wafuate *procedure* na wahakikishe kwamba wakipewa kibali wanakitumia kwa manufaa ya kile walichokiombea.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Susan Kiwanga atauliza swali.

Na. 180

**Hitaji la Kituo cha Polisi Mlimba**

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA** aliuliza:-

Kata ya Mlimba ni kubwa sana na hivyo kustahili kuwa Jimbo la Uchaguzi linalojitegemea:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Mlimba ili kuondokana na kero ya kuazima majengo ya *TAZARA* ambayo bado hayakidhi mahitaji ya Kituo cha Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan L. Kiwaga, Mbunge wa Viti Maluum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Kata ya Mlimba, Tarafa ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero, ni kubwa ikiwa na Kituo kimoja cha Polisi cha Tarafa kinachohudumia Kata saba, za Kamwene, Utengule, Kalengakero, Chisano, Uchindile na Masagati. Aidha, ni kweli kuwa Jeshi la Polisi linatumia jengo la

Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (*TAZARA)* ambalo halikidhi mahitaji ya kuhudumia ulinzi kwa tarafa hiyo yenye wakazi zaidi ya elfu arobaini, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa Vituo vya Polisi maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na Kata ya Mlimba aliyosema Mheshimiwa Mbunge. Azma hii njema ya Serikali inakwamishwa na ufinyu wa bajeti ya Serikali. Mara hali ya kifedha itakaporuhusu, maeneo yote yasiyo na vituo vyenye hadhi stahiki hapa nchini, yatapewa kipaumbele, ili kutoa huduma hii muhimu ya ulinzi na usalama kwenye majengo stahiki.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii muhimu kuwashukuru wananchi wa Tarafa ya Mlimba ambao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wameanzisha mchakato wa ujenzi wa kituo cha polisi na tayari eneo limepatikana na michango ya wananchi inaedelea kutolewa ili kuanza ujenzi wa kituo mapema iwezekanavyo. Huu ni mfano wa kuigwa na wananchi wa maeneo mengine yenye changamoto ya ukosefu wa vituo na nyumba za makazi ya askari wetu kama inavyofanyika kwa miradi ya shule, zahanati na maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga, swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu yaliyotoewa lakini kwa taarifa tu, kituo hiki cha Mlimba siyo kwamba kinahudumia tu tarafa zilizotajwa isipokuwa kinahudumia pia wananchi wa Wilaya ya Ulanga, kule Ngohelanga Malinyi, kinahudumia pia wananchi wa Wilaya ya Njombe kule Madeke – Lupembe lakini vilevile Mufindi, kule Mafinga wanahudumiwa na kituo hicho ambapo ni kilometa 25. Hali ni mbaya zaidi, wana pikipiki tu na kutoka kituoni mpaka huko magereza ni kilometa 150 kupeleka mahabusu lakini kibaya zaidi kina askari mmoja tu wa kike na hakina chumba cha mahabusu wa kike. Pamoja na ufinyu wa bajeti na wananchi kujitolea kujenga ninyi Serikali mnaunga vipi nguvu za wananchi katika kuharakisha kujenga kituo hicho ambacho kina hali mbaya sana? Hilo ndilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na kuwa Mlimba kuna matatizo lakini Wilaya ya Kilombero, hapo Ifakara kwenye Kituo cha Polisi cha Wilaya kiko karibu kabisa na mafuriko na maji yanaingia kila mwaka, hali ni mbaya kuliko kiasi na wanatumia majengo ya Maliasili, hivi, Kilombero tumekosa nini? Yaani Wilaya, majengo ya Maliasili, kule Mlimba majengo ya *TAZARA*, Serikali mnaweka kipaumbele gani katika Wilaya ya Kilombero kuhakikisha kwamba wana Kituo cha Polisi angalau cha Wilaya pale Ifakara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ina mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba vituo mbalimbali vya polisi ikiwa ni pamoja na kituo hiki cha Mlimba kinafanyiwa ukarabati. Mwaka huu katika bajeti ya maendeleo ambayo tumeipitisha hapa Bungeni tumetenga shilingi bilioni nane kipindi kilichopita kulikuwa na shilingi bilioni tano. Mara pesa hiyo itakapotoka kwa wakati Kituo cha Mlimba kitapewa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa mara nyingine kuwashukuru sana wananchi wa Mlimba ambao kwa jitihada zao wamechangia fedha na Kamati ya watu sita imeshaundwa ya kuanza mchakato huo. Mpaka sasa zimekusanywa takribani shilingi milioni tisa. Hivyo, Wizara inaahidi pesa ya bajeti itakapotoka, maana bajeti imeongezwa toka shilingi bilioni tano mpaka shilingi bilioni nane, kituo hiki cha Mlimba kitapewa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inaahidi kabisa kwamba eneo hili litazingatiwa na nimpongeze sana Mheshimiwa Susan kwa kuzingatia masuala ya ulinzi na usalama na kuunga mkono sera za Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Bado swali la pili.

**SPIKA:** La pili halikuwa kwenye swali la msingi, Mheshimiwa Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER-:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Ilumbwa wamejenga kituo kikubwa cha polisi na wamemaliza, tatizo ni nyumba za maaskari. Katika kila bajeti tunaambiwa kwamba ufinyu wa bajeti na kwamba tutapewa kipumbele bajeti ijayo. Je, Serikali sasa wanasemaje kuhusu nyumba za polisi katika kituo hicho cha Gelai Lumbwa.

**SPIKA:** Haya, kama anakijua sijui, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu wa kupanga bajeti ya maendeleo na matumizi mengineyo hapa Bungeni pia Wizara ya Mambo ya Ndani ina mpango wa kushirikisha wadau mbalimbali, mpango huu unaitwa *Public Private Partnership*. Maeneo mengi sana vituo hivi vimekuwa vikiendelea kujengwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Kuna mashirika, kuna makampuni ambayo tunaendelea kushirikiana nayo kuhakikisha kwamba suala la ulinzi na usalama kwa watu wetu ikiwa ni pamoja na makazi ya maaskari linafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo wako hata Wabunge ambao wameweza kushirikiana na Wizara hii ya Mambo ya Ndani kujenga kituo cha polisi, kwa mfano, Mheshimiwa Ritta Kabati kituo cha Semtema naye alijitahidi lakini kuna mashirika mengine, Shirika la *PPF*, *Konyagi Distillers*, *Twiga Cement*, tumekuwa tukishirikiana nao pamoja na Serikali lakini pia pamoja na wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba mara bajeti itakapotoka wakati utakapofika nyumba za askari za ile kata aliyoitaja zitapewa kipaumbele.

**SPIKA:** Haya, tuendelee na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura atauliza swali hilo. Nimesema Mheshimiwa Sabreena, yaani nyie hamsimami?

**MBUNGE FULANI:** Amesimama.

**SPIKA:** Alah, amesimama sijamuona, nani amesimama?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mkosamali.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mkosamali atauliza kwa niaba yake.

Na. 181

**Utaratibu Mpya wa Malipo ya Maduhuli Mahakamani**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Kwa mujibu wa utaratibu mpya wa malipo ya maduhuli yote Mahakamani yanapaswa kulipiwa benki ya *NMB*; utaratibu huo umeanza mwezi Aprili, 2015 kwa tangazo la Mtendaji Mkuu wa Mahakama lakini pamoja na nia hiyo nzuri utaratibu huu umegeuka kuwa kero kwa wananchi wa vijijini ambako hakuna huduma ya benki na pia hulazimika kulipa ada ya kuanzia Tsh.1,500 na kuendelea.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza kero hiyo kwa wananchi walioko vijijini?

**SPIKA:** *You are right,* swali linatoka Kigoma, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ADAM K. MALIMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama imeanza kukusanya maduhuli kwa njia ya kulipia kupitia benki. Lengo ni kupunguza malalamiko mbalimbali ya wateja hususan yanayohusiana na rushwa lakini pia kudhibiti upotevu wa fedha na kuongeza maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mahakama iliamua kutumia benki ya *NMB* kwa sababu hivi sasa ndiyo benki yenye mtandao mpana zaidi wa matawi kwenye wilaya zote nchini. Kwa kuwa ni takriban miezi miwili tu tangu mfumo huu wa kulipia ada umeanza kutumika kwenye maeneo hayo, Mahakama ya Tanzania inaendelea kufanyia tathmini changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa utaratibu huu wa malipo na kadiri matatizo ya mfumo huu yanavyobainika na hususan zile ambazo ni kero kwa wananchi tutatengeza utaratibu wa kuja na mapendekezo ya kuboresha mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kutambua utaratibu wa kufanya malipo kupitia benki imekuwa ni usumbufu kwa baadhi ya wananchi kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge na haswa wale ambao huduma za Mahakama zinapatikana kwenye sehemu ambazo hakuna huduma za kibenki za *NMB*, hivi sasa tayari tathmini imeshaanza ya kuboresha mfumo wa malipo kwa kutumia mitandao ya simu. Kwa kuzingatia hilo, Mahakama ina lengo la kupanua wigo wa kufanya malipo kwa kutumia njia mbalimbali za kielektroniki ambapo mhusika ataweza kufanya malipo mahali popote alipo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali maswali ya nyongeza.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Swali la kwanza, kwa kuwa suala hili limeonekana ni usumbufu, mtu kulipa Sh.1,500 au Sh.2,000 kwenda benki ni usumbufu, kwa nini utaratibu wa zamani usiendelee mkiwa mnaendelea na hizo taratibu nyingine unazosema yaani vifanyike vyote viwili kwa pamoja kwa sababu tayari ni kero sasa?

Mheshimiwa Spika, pili, huu utaratibu wa kutumia mitandao ya simu na vitu vingine utakamilika lini, kwa sababu ni jambo ambalo ni jepesi? Sasa hivi malipo kupitia simu ni jambo ambalo linafanywa na taasisi nyingi wala halihitaji tathmini za muda mrefu. Itachukua muda gani kwa Mahakama kuanza jambo hili?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ADAM K. MALIMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba huu utaratibu wa kulipa kupitia benki lengo lilikuwa ni kupunguza adha iliyokuwa inapatikana na upotevu wa maduhuli ya Serikali. Kwa sasa hivi, kwa sababu utaratibu huu umeanza kama miezi miwili tu iliyopita, kuna baadhi ya maeneo ambayo *NMB* kama haipo na huo uongozi wa Mahakama umeamua utaratibu huo usianze kwanza. Kwa hiyo, utaratibu huu umelenga kwenda kwenye maeneo ambayo kuna matawi ya *NMB*. Hata hivyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mkosamali moja kwa moja kwamba hata pale ambapo kuna tawi la *NMB* kwenda Mahakamani kwenda kupata ada ya Sh.1500 au Sh.2,000 halafu unatoka kwenda kwenye tawi la *NMB* kulipa halafu unarudi tena, nayo imekuwa ni kero.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi huu utaratibu wa *electronic payments* ambao tuliupitisha hapa kwenye Bunge lililopita ndiyo tunaoufikiria kwenda nao sasa hivi, ni kuoainisha mtandao pamoja na Mahakama na maeneo mbalimbali ili ukifika kwenye simu u-*click* upate malipo ya Mahakama uweze kulipia. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba utaratibu huu ufanyiwe kazi na nadhani utafanyika haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Shekifu.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nzuri za Serikali kutatua tatizo hili la kutumia fedha kupitia mtandao na mabenki, lakini liko tatizo la muda mrefu ambalo ni kero pia kuhusu ukosefu wa Mahakimu pamoja na wananchi kwenda masafa marefu kwenda kutafuta haki.

Serikali inachukua hatua gani baada ya kuunda Chuo cha Mahakama Lushoto kutatua tatizo la Mahakimu kupatikana kwa wingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. ADAM K. MALIMA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli, mwaka wa jana kwenye bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria zilitengwa pesa kwa ajili ya ajira ya Mahakimu 300 lakini katika mchakato mzima walipatikana Mahakimu watano tu. Kwa hiyo, mwaka huu pesa hizo zimetengwa upya kwa ajili ya ajira ya wafanyakazi kama 1,500 hivi katika sekta nzima ya Mahakama lakini kwa Mahakimu peke yake bado mkakati ni kuajiri wale Mahakimu 295 ambao walikusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi kuna mkakati wa ukarabati na ujenzi wa Mahakama mpya katika hatua zote. Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya zote na pesa zilizotengwa kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 20.5. Matarajio ni kwamba Wizara ya Fedha itahakikisha kwamba pesa hizo zinapatikana kwa sababu ya kuanza mchakato wa ama kwenye maeneo ya ujenzi kuanza ujenzi, lakini kwenye ukarabati wa Mahakama hizo uanze. Niseme tu kwamba mkakati huu unahusu mikoa na wilaya nyingi za Tanzania ukihusisha ujenzi vituo kama 40 hivi.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa John Lwanji, kwa niaba yake Mheshimiwa Kapt. Chiligati.

Na. 182

**Ahadi ya *REA* Kupeleka Umeme Manyoni**

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI (K.n.y. MHE. JOHN P. LWANJI)** aliuliza:-

Serikali kupitia *REA* iliahidi kupeleka umeme Mwamagembe katika mpango wake wa Awamu ya Pili *(Phase II)* Wilayani Manyoni:-

Je, ni lini mpango huo utatekelezwa ili wananchi wa Mwamagembe wapate umeme kabla ya Juni, 2015 kama ilivyoahidiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme katika kijiji cha Mwamagembe, Tarafa ya Itigi unatekelezwa na mkandarasi anayeitwa *CHICO* kutoka China na upo chini ya *lot* namba 24 ya Mkoa wa Tabora ambapo ilionekana itakuwa rahisi kupata umeme kutoka Kijiji cha Mitundu, Wilaya ya Sikonge. Mradi huu utanufaisha vilevile Vijiji vya Kalangali, Kiombo, Madoletisa, Kirumbi, Mwamagembe na Mwamalugu. Kazi ya mradi inahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilometa 65, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa kilometa 8.5, ufungaji wa *transformer* 16 na kuwaunganisha umeme wateja wa awali wapatao 227. Gharama ya upelekaji umeme katika vijiji hivi ni shilingi bilioni 1.28.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia sasa, utekelezaji umefikia asilimia 25 na mkandarasi anaendelea kufanya kazi katika vijiji vya upande wa Wilaya ya Sikonge na atamaliza katika vijiji vya upande wa Wilaya ya Manyoni hivi karibuni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapt. Chiligati maswali la nyongeza.

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza ningeomba *Hansard* ifanye masahihisho kwenye jibu la Mheshimiwa Waziri kwa sababu kijiji cha Mitundu hakipo Wilaya ya Sikonge, kipo Wilaya ya Manyoni. Kwa hiyo, naomba kumbukumbu za Hansard ziripoti vizuri jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya sahihisho hilo, nina maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, jibu linasema mpaka sasa mkandarasi huyu *CHICO* bado yuko katika vijiji vya Wilaya ya Sikonge na watu wa Mwamagembe waliahidiwa kwamba ifikapo Juni wangepata umeme, mkandarasi hajaonekana, sasa ni lini hasa watu wa Mwamagembe watarajie kazi hiyo kuanza pale Mwambagembe?

Mheshimiwa Spika, la pili, mradi wa kutoka Manyoni kwenda Tarafa ya Nkonko hadi Isanza umesimama sasa kwa karibu miezi mitatu. Hata Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea eneo lile mwezi Aprili walikuta mradi umesimama. Je, Wizara inasema nini kuhusu kusimama kwa mradi huo na utaanza kutekelezwa lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, nilipotembelea Wilaya ya Manyoni nilianzia Jimboni kwa Mheshimiwa Chiligati baadaye tukaenda Jimbo la Manyoni Magharibi. Pamoja na kwamba inaonekana kama mradi umesimama, nimhakikishie tu kwamba haujasimama, mkandarasi yuko upande wa Tabora na alikuwa ana-*mobilize* vifaa. Tuseme tu kwamba katika miradi hii ya ujenzi kazi kubwa zaidi ni *mobilization*, kupata vifaa na kuvileta *site*. Sasa hivi vifaa vipo *site*, nimhakikishie tu kwamba ujenzi utakamilika kama ambavyo tumeingia mkataba na mkandarasi huyu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Chiligati si kwamba umesimama bali ni kama nilivyosema kwamba *mobilization* ilikuwa inaendelea na mkandarasi ataendelea na asiwe na wasiwasi tutakamilisha kama ambavyo tumepanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii. Jimboni kwangu kuna mradi wa umeme unaofadhiliwa na kampuni ya *ORIO*…

**SPIKA:** Hatuna hakika hata Jimbo lenyewe linaitwaje.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu Jimbo la Mpanda Vijijini, yupo mkandarasi *ORIO* ambaye amepewa Vijiji vya Kabungu, Mchakamchaka, Ifukutwa na Majalila. Mpaka sasa mradi huu haujaanza, ni lini mradi huu utaanza? Naomba nipate majibu ya msingi.

**SPIKA:** Lakini swali siyo la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kakoso amenifuata na tumeongea kuhusu mradi huu wa *ORIO* ambao unajumuisha eneo lake pamoja na maeneo mengine ambayo anayatambua kabisa, likiwepo eneo la Mheshimiwa wetu Magufuli kule Chato. Mradi sasa hivi tayari tumeshapata hela, jenereta zinakuja na zitakapofika tutaendelea kusambaza umeme katika maeneo yote hivi karibuni. Nimuombe tu Mheshimiwa Kakoso awe na subira wakati uagizaji wa mitambo unaendelea ili ikishafika tu ataona na tutakwenda kwa kasi ambayo yeye mwenyewe atashangaa.

**SPIKA:** Hataamini? Mheshimiwa Lediana Mngo'ng'o. *(Kicheko)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kusambaza umeme na sasa hivi nguzo nyingi zimesimamishwa ikiwemo katika Wilaya ya Iringa na Mkoa wa Njombe. Je, ni lini maeneo yote ambayo nguzo zimesimamishwa umeme utaanza kuwaka ili wananchi waweze kufaidi huduma za umeme?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri jibu maswali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, nina hakika kabisa hata Jimboni kwako watu watakuwa wameshaanza kutokana na huu mradi wa kutoa umeme kutoka Makambako kuelekea Njombe. Katika maeneo yote kama alivyosema kwamba ukishaona nguzo zimesimamishwa maana yake wataweka waya na wakishamaliza kuweka waya wataweka *transformer* na wananchi watafungiwa umeme. Kwa hiyo, ni katika hali ya kawaida ya kuhakikisha kwamba huu mradi unatekelezwa na kwa jinsi wanavyotekeleza, wanaanza kwanza kuleta vifaa pamoja na nguzo, nguzo zinasimikwa wakishamaliza kusimika nguzo wanaleta nyaya,

wakishamaliza nyaya wanaleta *transformer* na wanasambaza kwa wananchi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwani tunaendelea na tutahakikisha kwamba watu wote wanafungiwa umeme kama ambavyo tumejipanga.

**SPIKA:** Ahsante. Tuelekee Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Anastazia James Wambura.

Na 183

**Upungufu wa Wataalamu wa Mionzi *(Radiologists)***

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Zipo taarifa kuwa kuna upungufu wa wataalamu wa mionzi *(radiologists):-*

(a) Je, kuna wataalamu wangapi katika nchi yetu?

(b) Je, masomo ya kozi hiyo ni muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kukabili changamoto ya upungufu wa wafanyakazi katika kada ya mionzi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeendelea kuendesha mafunzo ya kada hii katika ngazi za astashahada, stashahada na stashahada ya juu hapa nchini ingawa wahitimu watarajali wamekuwa wachache ukilinganisha na idadi ndogo ya vyuo vyenye uwezo wa kutoa mafunzo haya.

Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, jumla ya madaktari bingwa wa mionzi *(radiologists)* walikuwa 59 kwa nchi nzima, madaktari wasaidizi wenye stashahada ya juu ya radiolojia walikuwa 47, maafisa wa teknolojia radiografa yaani wenye shahada walikuwa 40 na wa teknolojia radiorojia/radiografa yaani wenye stashahada *(radiographic technologist)* walikuwa 408 na wa teknolojia radigrafa yaani waliokuwa katika ngazi ya astashahada walikuwa 22, hivyo jumla ya wataalamu wote wenye kada katika ngazi hii walikuwa 517 na madaktari bingwa 59.

(b) Mheshimiwa Spika, sambamba na kuboresha mafunzo na pia kuendana na Mpango wa Afya ya Msingi, Wizara imepitia mitaala mbalimbali ya mafunzo kulingana na mabadiliko katika sekta ya afya kwa nia ya kuboresha mafunzo. Wahitimu wa mafunzo hayo wanatoa huduma bora kulingana na mahitaji halisi ya afya kwa wananchi. Muda wa mafunzo kwa wataalamu hawa unapishana kulingana na kiwango cha utaalamu unaotakiwa, mafunzo ya ngazi ya shahada ya uzamili huchukua miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu huu, Wizara imepitia mpango wake wa kuzalisha watumishi wa Sekta ya Afya *(Production Plan)* wa miaka kumi 2014-2024 na imepanga kuzalisha wataalamu watarajali ambao watakidhi mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili linatokana na mikakati ambayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufufua na kuboresha miundombinu ya vyuo vilivyokuwa vinatoa mafunzo hayo;

(ii) Kukarabati na kupanua baadhi ya vyuo ili kuongeza uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi zaidi;

(iii) Kutenga na kuongeza ruzuku kwa vyuo vya mashirika ya dini ili kuviwezesha kudahili wanafunzi zaidi kuliko ilivyo sasa; na

(iv) Kutoa ajira kwa wahitimu wote wanaotarajiwa kuhitimu katika vyuo vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pia naipongeza sana Serikali kwa kuonyesha jitihada za kuongeza wataalamu wa mionzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhaba au upungufu wa wataalamu wa mionzi lakini upo upungufu mkubwa sana wa huduma hizi za mionzi katika nchi yetu na hasa katika Mkoa wetu wa Mtwara. Hili limepelekea wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kwa kusimamiwa na kuhamasishwa na wawakilishi wao wa Chama cha Mapinduzi kununua wao wenyewe mashine ya *Ultra Sound*. Napenda kujua, je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza huduma za mionzi katika nchi yetu na hasa katika Mkoa wa Mtwara?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wapo wananchi au watu mbalimbali ambao wanajitolea kupeleka vifaa vya mionzi katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, mimi mwenyewe niliwahi kupeleka mashine ya *Ultra Sound* katika hospitali moja ya Wilaya kule Mtwara lakini kukawa na tatizo la kukosekana kwa mtaalam wa kuitumia. Pale kulikuwepo na daktari wa *volunteer* mmoja ambaye aliwafundisha madaktari wengine ndani ya muda mfupi wakaanza kuitumia mashine hii. Vilevile, niliwahi kupeleka mashine ya *electrocardiography* pale Ligula ili iende katika moja ya Wilaya. Pakawa na shida kwamba hakuna wataalamu katika Wilaya yoyote ikabidi ile mashine ibaki pale Ligula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, ni kwa nini Serikali imeondoa haya mafunzo ya astashahada ambayo nadhani wahitimu wake wangesaidia sana katika maeneo ambayo yana upungufu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ni mkakati gani ambao Serikali tunao, kama nilivyoeleza, wanafunzi watarajali tunatarajia wataongezwa kadri miaka inavyokwenda katika hiyo *plan* ya *production* ya 2014-2024 ili kusudi tuweze kuongeza watumishi. Hiyo ni sambamba na Mpango wa Afya ya Msingi yaani *MAM* ambapo watumishi wameongezeka sana. Wakati Awamu hii ya Nne inaingia madarakani kulikuwa na watumishi wa afya wapatao 56,000 lakini katika miaka 10 iliyopita sasa tuna watumishi wa afya takribani 82,000. Kwa hiyo, kazi ya kuongeza wataalamu wa afya ni pamoja na juhudi zote hizi ambazo zinaendelea pamoja na hiyo *production plan* wataalamu hao wataongezwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ameuliza kwamba, ni kwa nini mafunzo ya astashahada yaliondolewa. Katika mpango ambao tumeupitia sehemu hii imejumuishwa na ndiyo sababu wanafunzi watarajali, suala ambalo halikuwepo, sasa hivi tunaongeza zaidi na kuongeza fursa katika *training* kwa wadau mbalimbali yakiwemo mashirika ya dini ili iweze kwenda sambamba na ndiyo sababu tumeongeza vilevile katika suala zima la *BRN* yaani Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa. Kipaumbele cha kwanza kabisa ni jukumu la kuongeza wataalamu hawa pale ambapo hawapo. Tumetazama kwa nchi nzima yapo maeneo mengine kwenye Watanzania 10,000 wanakuwa *served* na wataalamu wenye sifa stahili watatu au chini ya saba, wastani ule kwa kweli haukidhi viwango kulingana na *WHO standards.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili litatazamwa katika mtazamo huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo ya kitaalamu sana aliyoyatoa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya ndani ya Bunge na uhalisia wa mambo nje ni vitu viwili tofauti. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anayo habari kwamba katika zile hospitali muhimu kama ya Muhimbili wananchi wengi wakienda wanapata shida sana kupata huduma hizi? Hata hivyo, wahudumu walewale au wataalamu walewale wa Muhimbili wakienda katika hospitali za *private* unawakuta na wanakupa huduma bila matatizo. Hivi tatizo ni nini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika Hospitali ya Muhimbili tulishatoa maelekezo kwamba huduma ya afya ipatikane mapema iwezekanavyo. Kwa hiyo, mtu kutoka Muhimbili kwenda sehemu nyingine mara nyingi ni suala la mtazamo na mapenzi ya mtu binafsi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Wakati mwingine anapenda apate huduma kwa haraka na kutokana na msongamano ilivyo pale Muhimbili inasababisha watu kupenda kwenda sehemu nyingine.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala hili tumelitazama kama ifuatavyo. Katika Hospitali za Rufaa zote kuu nne tulizonazo na ya tano tunaendelea kuijenga kule Mtwara, hospitali zote hizi hivi karibuni zitapata *CT-scan* pamoja na *X-Rays* za dijitali. Ndiyo sababu tumetoa maelekezo kwa nchi nzima kwa Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa na hospitali nyingine zote za rufaa maalum wafunge mtandao wa elektroniki ili kusudi vifaa hivi vinapokwenda katika mradi ambao tumeingia makubaliano na Serikali ya Uholanzi, tumeshapata shilingi bilioni 4.1 wakati wowote tutalipa hiyo *matching fund* ili kuongeza huduma hii ya radiolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napeda kumwambia Mheshimiwa Khalifa asiwe na wasiwasi kwani huduma hii inaboreshwa zaidi. Pia Hospitali ya Bugando itapata *MRI*, vipimo vya kisasa kabisa, ndiko tunakokwenda. Ndiyo sababu tumehimiza hospitali zote nchini waweke mtandao wa elektroniki, vifaa hivi vinapokwenda kazi ifanyike kwa utaalamu wa kisasa. Tunashukuru Mheshimiwa Zungu wakati anachangia Wizara ya Afya alisema unapigwa picha halafu unaweka kwenye *USB* au kwenye *CD* unakwenda nayo sehemu

yoyote. Kwa hiyo, tutafika mahali kama ilivyo baadhi ya hospitali nyingine, inapigwa *X-ray* inasomwa kulekule wodini siyo kukimbia tena na *film* imeshapitwa na wakati.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Wizara ya Elimu na Mafunzo Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 184

**Kutoza Ada kwa Fedha za Kigeni-Vyuoni**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni shule ngapi na vyuo vya elimu hapa nchini ambavyo vimeruhusiwa kutoza ada kwa fedha za kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Ernest Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu hapa nchini unaongozwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ambayo hutoa mwelekeo wa elimu nchini. Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, kifungu cha 3.6.2 kinaelezea kuwa Serikali itaweka utaratibu wa ada na michango mbalimbali katika shule na vyuo binafsi ili kusimamia ufanisi wa masuala ya ada na michango mbalimbali katika shule na vyuo.

Mheshimiwa Spika, Nyaraka na Miongozo ya Elimu iliyowahi kutolewa na Kamishna wa Elimu kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sera kwa ufanisi, haijawahi kutoa kibali cha kutoza ada kwa fedha za kigeni kwa shule au vyuo vya ualimu. Kwa mfano, Waraka wa Elimu Na.10 wa mwaka 1998 unaoruhusu mabadiliko ya ada kwa shule na vyuo vya ualimu vya binafsi na Waraka wa Elimu Na. 19 wa mwaka 2002 unaoruhusu ongezeko la ada kwa shule zisizo za Serikali zilizotoa viwango vya ada kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu vya binafsi vya kwa fedha ya Kitanzania kwa kuzingatia kuwa utoaji wa elimu ni huduma na si biashara. Lengo ni kumwezesha kila Mtanzania kupata elimu stahiki bila kikwazo.

Mheshimiwa Spika, utozaji wa ada katika vyuo vikuu hudhibitiwa na Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU)*. Viwango vya ada vinavyotakiwa kutozwa ni kwa fedha ya Kitanzania tu. Hata hivyo, napenda kukiri kwamba baadhi ya shule/vyuo vilikuwa vinakiuka maagizo ya Serikali na kutoza ada kwa fedha za kigeni.

Mfano, Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala *(Kampala International University)* na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia *(International Medical & Technological University-IMTU)* wamewahi kutoza ada kwa wanafunzi wa Kitanzania kwa fedha za kigeni na Tume ya Vyuo Vikuu ilipopata taarifa uongozi wa vyuo hivyo uliagizwa kusitisha utaratibu huo mara moja.

Mheshimiwa Spika, zipo shule zilizoanzishwa kwa ajili ya kuhudumia watoto wa Mabalozi, Maafisa wa Ubalozi na wafanyakazi kutoka Mataifa ya nje walioko nchini. Shule hizo hutumia mtaala wa Kimataifa unaojulikana kama *International Baccalaureate (I.B)* na hutoza ada kwa fedha za kigeni. Shule zinazotoza ada kwa fedha za kigeni ni pamoja na *Dar es Salaam International Primary School, International School of Tanganyika, Heaven of Peace International School na Laureate International School and Education Trust Fund.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, maswali ya nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitembelea katika nchi nyingi tu za wenzetu na tumeona kwamba huduma nyingi sana zinatolewa kwa fedha ya nchi husika. Katika jibu la msingi la Serikali imekiri kuwa haijawahi kutoa kibali cha kutoza ada kwa fedha ya kigeni kwa shule na vyuo. Hata hivyo, bado kuna shule nyingi tu za Kimataifa *(international schools)* ambazo hazina kibali zimekuwa zikitoza ada kwa fedha ya kigeni na zimekuwa zikikiuka hilo agizo ambalo limetolewa na Serikali. Naomba Mheshimiwa Waziri leo hii atoe kauli ya Serikali kuhusiana na hizo shule ambazo hazijapewa kibali cha kutoza fedha za kigeni na bado zinaendelea kutoza ada kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali kupitia *TCU* ilikuwa inafanya ulinganifu wa ada katika vyuo vikuu vya Serikali na vyuo vikuu vya binafsi ili kuhakikisha kwamba ada hizo hazipishani sana na hali hii inaashiria kuwa kuna vyuo vikuu vinavyotoza ada ya juu kuliko ada nyingine. Ukichukulia mfano Chuo cha Dar es Salaam, unaona wanatoza Sh.1,000,000/= na labda Chuo cha *RUCO* wanatoza zaidi ya hiyo Sh.1,000,000/=. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa sababu utakuta watoto wa wazazi wasiojiweza wanashindwa kwenda kwenye…

**SPIKA:** Sasa badala ya swali inakuwa hotuba.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Naomba kauli ya Serikali kuhusiana na ulinganifu wa hizo ada kwa vyuo vya Serikali na *private*.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza swali lake la kwanza kuhusu shule nyingine kuendelea kutoza ada kwa fedha za kigeni zozote zile ambazo si fedha za Tanzania, nilishajibu swali hili hapa Bungeni lakini leo naomba nitoe msisitizo. Kama tukithibitisha kwamba kuna shule zinazoendelea kukiuka sheria ya nchi ya kutoza ada kwa *Tanzanian shillings* na kwenda kutumia aidha pesa za Kiingereza au Kimarekani, shule hizi tutazichukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuzifungia shule hizo. Swali la kwanza naomba nilijibu hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba nikiri kwamba, hivi vyuo vimekuwa vinatofautiana sana katika kutoza ada na hasa vyuo vikuu. Kama ukiangalia Muhimbili *course* ya udaktari inatoza takribani Sh.1,800,000/= lakini ukienda chuo kikuu kama Herbert Kairuki yeye *school fees* yake ni takribani shilingi milioni tatu na zaidi. *TCU* ilishamaliza kukokotoa na kutuletea Wizara ya Elimu mfumo wa ada elekezi na sisi Wizara ya Elimu tumewarejeshea *TCU* ili waangalie athari upande wa bajeti. Wakishaturejeshea tutatoa rasmi ada ambayo ndiyo itatumika kwa vyuo vikuu vyote na itakuwa si vinginevyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Akunaay.

**MHE. MUSTAPAH B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kuiuliza Serikali kwa jumla kuhusu malipo ya huduma zinazotolewa hapa Tanzania kutozwa katika fedha za kigeni. Kwa mfano, Wizara ya Maliasili na Utalii kutaka watu walipe leseni kwa ku-*gauge* kwenye dola.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Akunaay.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitoa ufafanuzi muda mrefu kwamba kama tamko la mwaka 2007 lilivyokuwa likizungumza kwamba kuna huduma maalum ambazo zimeruhusiwa kufanyika kwa dola. Kwa mfano, hoteli ambapo *target* kubwa ni wageni na tulikuwa tunataka wawe wanaweza kulipia kwa dola lakini haimaanishi kwamba hawawezi kulipia kwa shilingi za Tanzania *as long as rates* zinakuwa zinaonyeshwa. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni tamko la mwaka 2007 na linaendelea hadi leo. Cha msingi ni kwamba, Mtanzania yeyote halazimishwi wala asilazimishwe kulipia kwa dola huduma yoyote, anaweza kulipia kwa shilingi.

Mheshimiwa Spika, zile sehemu ambazo zinataka kutumia dola au zinakuwa-*required* kutumia dola, kwa mfano, *international schools* ambazo *target* kubwa ilikuwa ni wageni, ni lazima *rates* zionyeshwe kwa *Tanzania shillings* ili hata kama wakitaka kulipia kwa shilingi ya Tanzania wanaweza kufanya hivyo. Hakuna huduma ambayo inamlazimisha mtu kutumia dola akitaka anaweza kutumia shilingi vilevile na tumekuwa tukilisisitiza hili.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa muda umekwisha na maswali yameisha.

Naomba niwatambue baadhi ya wageni ambao nimepewa majina yao. Nina Naibu Kamishna wa Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Tanzania - *DCP* Adolfina Chialo, naomba asimame popote alipo. Ahsante sana kwa kazi nzuri unayoifanya. *(Makofi)*

Tuna Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Mkoa wa Dodoma, Afande Hamda Hiki. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mwezeshaji wa masuala ya jinsia kutoka *TGNP,* Ndugu. Donald Bwire Donald. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mwezeshaji, Afande Manyama Wambura. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunawashukuru sana kwa juhudi zenu za kuweza kusaidia watoto na akinamama wanaoteseka kwa namna moja au nyingine katika shughuli zenu.

**MBUNGE FULANI:** Na akinababa.

**SPIKA:** Akinababa wana nguvu. *(Kicheko)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Lediana Mg'ong'o ambao ni Maaskari wa Jeshi la Polisi wanaosimamia Madawati ya Jinsia na Watoto kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma. Naomba hawa pale walipo wasimame. Kumbe ni Jeshi kubwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Ndugu Clement Sanga, mtangazaji wa C*hanel Ten* Mkoani Iringa. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe Steven kebwe, Naibu Waziri wa Afya ambaye ni Ndugu Deogratius Nyamange - Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Natta Serengeti. Ahsante, karibu. *(Makofi)*

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine - Morogoro wakiongozwa na Ndugu George Magway. Hawa na jana walikuwepo, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Halima Mdee kutoka shule mbalimbali za sekondari Dar-es-Salaam, wakiongozwa na Ndugu Evance Saul. Pale walipo wasimame, *okay*, naona wengine hawajaingia.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mchungaji Lukson Mwanjale ambaye ni Mchungaji Christopher Mwashiuya, kutoka Kanisa la Uinjilisti Mbalizi. Naomba muombee nchi, ahsante. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Tuna wanafunzi sabini na nne na walimu kumi na tatu kutoka *St. Gemma Galgan Pre and Primary School Arusha.* Naomba msimame wote na walimu, tumefurahi kuwaoneni. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna Taasisi ya Vijana 40 kutoka *Dodoma Youth Development*, yenye malengo ya kuwasaidia vijana kielimu, kiuchumi na kijamii wakiongozwa na Ndugu Rajab N'hunga. Naomba pale walipo wasimame. Ahsante sana, tunaomba muendelee kuwa na uadilifu katika mambo hayo. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Endrick Silali Yohana, huyu ni mwanafunzi kutoka shule ya sekondari ya Sogesca - Simiyu. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo mwisho wa matangazo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mwongozo Mheshimiwa Dokta Mrema, nimewaona na wengine tuanze.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kulingana na Kanuni ya 68(7). Juzi wakati wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi, nilichangia hapa nikaeleza matatizo makubwa yanayosabishwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Ndugu Gama kuhusu umilikaji wa shamba la Lokolova - Himo. Sasa hivi kuna mgogoro mkubwa, wananchi wana njaa lakini wamezuiwa kulima shamba lao tangu 2013, 2014 na 2015. Kuna Kata kumi na tano na zaidi ya wananchi elfu arobaini wanaohitaji chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipokuja Vunjo na kuzungumzia suala la Soko la Kimataifa, tulimuomba na tukampeleka Njia Panda akasema eneo ni dogo, tukampeleka Lokolova, wale wanaushirika zaidi ya 1,200, kwa

hiari na upendo wao kwa Rais wao wakakubali kumgawia heka 140 kwa ajili ya ujenzi wa soko la Kimataifa. Tena wakampa bure bila hata kulipia shilingi mia na heka moja pale Himo inauzwa shilingi milioni mia lakini kwa kumpenda Rais wakasema watampa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichojitokeza ni kwamba, wale wanaushirika walikuwa na heka 2,610 ukiondoa hizo 140 walizompa Mheshimiwa Rais, zikabaki heka 2,470. Mkuu wa Mkoa akatenga heka 2,000, akafanya *Memorandum of Understanding* na *TIB* kupata mkopo kwa kuweka zile heka elfu 2,000 rehani bila kibali cha wanaushirika ili hilo soko la Kimataifa …

**SPIKA:** Usigeuze suala la mwongozo kama hotuba.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, namalizia. Ili aweze kuchukua zile heka 2,000 akafuta ule ushirika wa kilimo na ufugaji, jambo hili ni tete.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuta ule ushirika yeye akaunda Kampuni ya *Kilimanjaro Uchumi Company Limited* ya kuendesha soko lile bila ya kibali cha wanaushirika. Wanaushirika wale wamelalamika, tumekwenda kwa Rais na Waziri Mkuu, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa hekima zake na nashangaa mpaka leo hajachukua fomu ya Urais sijui anangojea nini kwa sababu alitumia hekima akaamua kurejesha ile hati ya ushirika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza pale ni kwamba, ule ushirika tuliokuwa nao umerudi kwa wananchi. Wanachosema ambacho wanakilalamikia, *role* ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa tumemwita ni dalali wa mashamba, ni dalali wa viwanja, siyo kwamba tunamwonea au tunamkashifu.

**SPIKA:** Naomba ufupishe.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema naomba kauli ya Serikali, tunafanyaje pale kwenye ule ushirika wa Lokolova? Mbona tunagombana na Mkuu wa Mkoa wakati mashamba yale ni yetu sisi wanaushirika na viwanja vile ni vyetu. Kama kuna mbia tuna uwezo wa kuingia naye kwenye ubia huo na kama tukiamua kuuza viwanja au mashamba hayo tunauza wenyewe, Mkuu wa Mkoa ametokea wapi kwa nini anafanya biashara na wakati mmesema Serikali haifanyi biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni hilo naomba mwongozo wako.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nikishasimama huwezi kunipa taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa makini sana siku ile wakati Wizara hii inaendelea. Suala la tuhuma zilizokuwa kwa Mkuu wa Mkoa alizitoa Halima kwanza, likaungwa mkono na wengine pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mrema. Nilivyomsikia Waziri alisema kwamba wanaenda kutafuta habari hizo, kwa sababu kumtuhumu mtu katika kiwanja kikubwa kama hiki halafu hamna uhakika siyo sahihi. Nitakachokifanya ni kwamba, maelezo haya kabla ya kumaliza hili Bunge wawe wametoa, nadhani muda unatosha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kuhusu swali langu ambapo niliuliza swali la msingi na maswali mawili ya nyongeza lakini la pili kuhusu ujenzi wa Kituo cha Wilaya ya Polisi ya Kilombero - Ifakara halijajibiwa kabisa na kipo kwenye hali mbaya sana.

**SPIKA:** Si wamekuambia wanazo pesa wataviangalia hivyo vituo? Mheshimiwa Mussa Kombo.(Kicheko)

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kutumia Kanuni ya 68(7).Naomba mwongozo wako kwenye swali namba 183 ambalo limeulizwa muda mfupi sana uliopita. Mheshimiwa Khalifa ameiuliza Wizara ya Afya, wagonjwa wanapokwenda hospitali za Serikali kama Muhimbili na nyingine wanacheleweshwa au hawapati huduma lakini madaktari walewale wanapokwenda hospitali za nje ambazo wanazifanyia kazi huwa wanawahudumia haraka sana.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha ni kwamba, Waziri hakutoa majibu ya kuridhisha kwa suala ambalo linahusiana na maisha ya binadamu na mali zetu na jinsi hospitali zetu zinavyoendeshwa. Ni kweli wagonjwa wanapokwenda katika hospitali za Serikali wanapata matatizo makubwa, lakini wao madaktari ndiyo wanaoongoza, nenda hospitali hii, kanunue dawa duka hili.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa nini Serikali inatudanganya na hawataki kuwa wakweli juu ya maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunao ule mradi wa *Legislative Support Programme*. Moja ya kazi ambayo tutamaliza kipindi hiki hatukufanya, tulitaka tufanye utafiti wa kutosha ni namna gani tunaweza kuhuisha matibabu katika hospitali za Serikali na za watu binafsi. Kwa sababu nchi nyingine kama India hata tunapokwenda Apollo siyo za Serikali, lakini kwa nini sisi inakuwa ni tatizo?

Hiyo ndiyo ilikuwa kazi ambayo tulitakiwa tuifanye, lakini bahati mbaya tunamaliza muda. Hata hivyo, ile *programme* ya *Legislative Support* itaendelea tena kwa awamu nyingine. Ni suala kubwa la kuliangalia siyo dogo ni pamoja na hivi vitu vinaitwa *insurance* ya afya, ni muhimu.

Wenzetu wananchi wao wanaweza kwenda hospitali yoyote ile hata Apollo kwa sababu *insurance* yao wanatibiwa mahali popote. Kwa hiyo, suala la madaktari kuhama kutoka hospitali za Serikali kwenda kwa watu binafsi linakuwa halina maana yoyote. Hili suala tunaliachia Bunge la Kumi na Moja kufanya utafiti kwa nini sisi iko namna hii?

Mheshimiwa Machangu ulisema taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba nimpe Mheshimiwa Mrema taarifa ya Lokolova.

Mheshimiwa Spika, tulikaa vikao vyote halali, Mkuu wa Mkoa alifanya vikao vyote halali na tulikaa kwenye *RCC* na kila kikao tukakubaliana. Hapa Mheshimiwa Mrema anatafuta kura za wana Vunjo, naomba asitumie suala hilo kwa ajili ya kutafuta kura.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**SPIKA:** Ningekuwa nimejua ni taarifa hiyo unataka kutoa nisingekupa nafasi. (*Kicheko)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, mimi ndiyo Mbunge halali wa Vunjo. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Kama nilivyosema Wizara ya Ardhi, ndivyo ilivyoahidi siku ile.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuzungumze mambo yetu. Kesho ndiyo siku ambayo itasomwa bajeti lakini asubuhi tutafika kama kawaida maswali halafu Waziri anayehusika na mambo ya Mpango atawasilisha mpango wa nchi. Hatutakuwa na maswali ya Waziri Mkuu kwa sababu ukiyaweka yatachukua picha kuliko bajeti inayosomwa siku hiyo. Kwa hiyo, kesho asubuhi hatutakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, nawaombeni sana saa kumi tutakuwa na wageni wengi, kwa hiyo nawategemea na ninyi mtakuwa nadhifu maana hizi rangi tulizovaa leo zimezidi. Rangi hizi ni nyingi mno, kuna nyekundu na rangi ningine, siku ya bajeti watu wanavaa rasmi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 11 Juni, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*